

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

634


STADI ZA KAZI

Muda: Saa 3

Mwaka: 2022

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na nne (14)**.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Soma maelekezo **yote** katika kijitabu chako cha kujibia.
5. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Kwa kutumia maarifa uliyojifunza katika uchambuzi wa muundo wa Muhtasari wa somo la Stadi za Kazi, ainisha taarifa nne muhimu zinazopatikana katika ukurasa wa haki miliki.
2. Umepeleka nguo yako kwa fundi cherehani kwa ajili ya kudarizi. Ni mambo gani ya msingi fundi huyo anapaswa kuyazingatia kabla ya kufanya kazi hiyo? Toa hoja nne.
3. Kwa kutoa hoja nne, bainisha mbinu zinazoweza kutumika katika kufundisha mada ya ufugaji wa bata kwa wanafunzi wa Darasa la Nne.
4. Ni vyanzo gani vinaweza kutumiwa na mfanyabiashara mdogo kupata fedha za kununulia mtaji? Bainisha vyanzo vinne.
5. (a) Eleza kwa kifupi dhana ya Zana za Kufundishia na Kujifunzia kama inavyotumika katika somo la Stadi za Kazi.
(b) Bainisha faida tatu za kutumia dhana ulioieleza kwenye 5 (a) katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi.
6. Kuna umuhimu gani wa kupitisha pasi kwenye kitambaa cha kujaribia kabla ya kuanza kupiga pasi nguo? Eleza kwa kifupi kwa kutoa hoja mbili.
7. Mtaalamu wa mifugo katika hotuba yake alisisitiza umuhimu wa kudumisha afya njema ya ng'ombe wa maziwa. Kwa kutumia hoja nne, eleza kwa ufupi msingi wa msisitizo huo.
8. Bwana Ambindwile ameteuliwa kughani shairi katika maadhimisho ya siku ya wanawake duniani. Je, anatakiwa azingatie mambo gani wakati wa kughani shairi mbele ya kadamnasi hiyo? Ainisha mambo manne.
9. Umealikwa kuwafundisha washiriki wa mashindano ya kuimba ya *Bongo Star Search*. Bainisha mbinu nne utakazowaelekeza ili waweze kuimba vizuri.
10. Umepewa jukumu la kuwafundisha wanafunzi wa Darasa la Nne namna ya kuigiza kwa kutumia onyesho mbinu. Chambua kwa kifupi faida nne za kutumia mbinu hiyo.

SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

11. Ni kwanini ni muhimu kwa mkulima kutumia mbegu bora katika ustawishaji wa mboga shambani? Eleza kwa kutoa hoja sita.

12. Mkuu wa Shule ya Msingi Njinjo amekupa kazi ya kuwafundisha wanafunzi wa Darasa la Tano kuhusu upishi wa ugali. Eleza hatua sita utakazowaelimisha wanafunzi katika somo hilo.
13. Umahiri wa mwalimu ni pamoja na uwezo wake wa kuandaa na kutumia Andalio la Somo. Fafanua faida sita anazozipata mwalimu wa somo la Stadi za Kazi anapotumia Andalio la Somo wakati wa ufundishaji.
14. Mwalimu wa taaluma amewaagiza walimu wote kuandaa maswali ya kuchagua jibu sahihi kwa ajili ya kuboresha utungaji wao wa maswali shuleni. Fafanua kanuni sita wanayopaswa kuzingatia katika kunda maswali hayo.